# Jenista aipa maagizo bodi serikali mtandao

Na NASRA KITANA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameitaka Bodi ya Wakurugenzi iliyoundwa ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, kuhakikisha inazuia wizi, rushwa na matumizi mabaya ya mitandao.

Jenista aliyasema hayo jana, wakati wakati akiizindua bodi hiyo katika ukumbi wa Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza mara baada ya kuzindua bodi hiyo, Jenista alisema anaamini bodi hiyo, itasaidia kuondoa rushwa katika majukumu ya kila siku ya kuwahudumia wananchi.

Alisema dhamira ya serikali katika kupata ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za wananchi ni kuamua kufanya matumizi ya mtandao kwa ujumla, hivyo bodi hiyo, imeundwa iweze kusimamia ipasavyo.

"Kwanza, nashukuru bodi ambayo tumeiteua, imeweza kukubali kufanya kazi, hivyo nahitaji kuona wanapambana kuhakikisha wanazuia rushwa, wizi na matumizi mabaya ya mtandao, tuweze kutumia vyema," alisema Jenista.

Waziri huyo anaamini kuwa, bodi hiyo chini ya Mwenyekiti wake Dk. Mussa Kissaka na wajumbe wote walioteuliwa, watashirikiana kikamilifu na wizara kuhakikisha kuwa, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), inatumika kuboresha utendaji kazi ndani ya taasisi za umma na utoaji huduma.

Aidha, waziri Jenista, amempongeza Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi anazofanya kuhakikisha matumizi ya TEHAMA ndani ya serikali yanakua.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, alisema kuwa, wote wanafahamu serikali mtandao, pamoja na mambo mengine, inahimiza matumizi sahihi ya TEHAMA kama chombo kilichopewa jukumu la kusimamia serikali mtandao.

"Sisi kama mamlaka, tutahakikisha tunatoa ushirikiano wa dhati na serikali na kufuatilia kikamilifu maelekezo katika kusimamia utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao hasa za ujenzi wa miundombinu na mfumo shirikishi na ile ya kisekta kwa kushirikiana na taasisi za umma kwa kuzingatia kanuni na sheria," alisema Ndomba.

### MWENYEKITI WA BODI

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa bodi hiyo, Mussa Kissaka, alisema watahakikisha wanatekeleza majukumu yote waliyokabidhiwa na serikali, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapunguza changamoto ya rushwa na wizi mtandaoni.

Wajumbe wanaounda bodi hiyo mpya ni Angelista Kihaga, Priscus Kiwango, Eric Shitindi, Francis Kayichile, Aloys Mvuma, Justima Mashiba na Dk. Jasmine Tiisekwa.

MWONGOZO



ALIYEWAHI kuwa Waziri, Mhandisi Christopher Chiza (kushoto), akipokea kitabu cha Mwongozo wa Mwanachama kutoka kwa Meneja wa Kurugenzi ya Fedha ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma PSSSF, Michael Bujiba, katika Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha yanayoendelea jijini Mwanza, jana. (Na Mpigapicha Wetu).

# Wasambazaji vipuri vya magari, wamiliki karakana wafundwa

NA MWANDISHI WETU, Dodoma

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wauzaji, waagizaji, wasambazaji wa vipuri vya magari na wamiliki wa karakana za magari kutambua mwelekeo wa serikali ya awamu ya sita, ambayo imedhamiria kuendeleza sekta binafsi.

Limesema lengo kutoa ajira kwa kada mbalimbali na kuyawezesha magari yanayorekebishwa katika karakana nchini kukidhi matakwa ya viwango husika. Meneja wa TBS, Kanda ya Kati, Nickonia Mwambene, alisema hayo mkoani Dodoma, juzi wakati wa shirika hilo lilipokuwa likihitimisha mafunzo kwa washiriki hao wa mikoa ya Mwanza, Arusha na Dodoma.

Aliwahimiza washiriki kuwa na mwelekeo mzuri zaidi na wa kiuweledi katika kutekeleza matakwa ya viwango husika na huduma wanazotoa kwa jamii. Aliwataka washiriki kutambua mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita, ambayo imeazimia kwa dhati kuendeleza sekta binafsi, kutoa ajira kwa kada mbalimbali na kuyawezesha magari yanayorekebishwa katika karakana nchini kukidhi matakwa ya viwango husika. Meneja huyo alieleza mafunzo yamelenga sekta muhimu katika sekta binafsi inayochangia pato la taifa na kuongeza ajira. Alisema hiyo ni kutokana na azma ya serikali ya kuendelea kujenga uchumi wenye nguvu, imara na wenye ushindani, hivyo shirika linaunga mkono mipango na juhudi zote zinazofanywa kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zinakidhi matakwa ya ubora zikiwemo vipuri vya magari. Kuhusu mafunzo, meneja alisema yanalenga kuwaandaa washiriki kuwa wenye mwelekeo mzuri zaidi na wa kiuweledi kutekeleza matakwa ya viwango husika na huduma wanazotoa kwa jamii. Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa walengwa hususan kwa kuzingatia watumiaji ambao hutegemea sana waagizaji na wauzaji wa vipuri vya magari na wenye karakana, kuwashauri kuhusu aina na ubora wa vipuri sahihi vya magari.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, Ofisa Kilimo, Mkoa wa Dodoma, Bernad Abraham, alisema washiriki hao ni wadau muhimu katika sekta binafsi inayochangia pato la taifa, kuongeza ajira na wanasaidia kuondoa umaskini. Katika Mkoa wa Dodoma mafunzo hayo yalihudhuriwa na washiriki 25 ambapo Abraham alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati katika uwekezaji wa sekta binafsi, hivyo wauzaji wa vipuri vya magari na wamiliki wa karakana sehemu ya shughuli za uzalishaji kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo mkoani humo.

Alifafanua uongozi wa mkoa unaamini warsha hiyo ni njia mwafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuiletea taifa maendeleo ya haraka kulingana na fursa zilizopo hususan kwa sekta ya biashara na maeneo mengine.

Warsha

UMUHIMU

Alifafanua uongozi wa mkoa unaamini warsha hiyo ni njia mwafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuiletea taifa maendeleo ya haraka kulingana na fursa zilizopo hususan kwa sekta ya biashara na maeneo mengine.

# NMB yazipiga 'jeki' shule zilizobomolewa kwa kimbunga

NA MWANDISHI WETU, Kibiti

BENKI ya NMB imepaua shule zilizobomolewa na kimbunga na kufanya ukarabati wa madarasa, ofisi na nyumba za walimu wa shule za Msingi za Mlanzi, Ngondae na Mangombela zilizoko wilayani Kibiti, mkoani Pwani.

Nyumba hizo ziliezuliwa na kimbunga kikali kilichotokea Januari 20, mwaka huu.

Akikabidhi msaada wa vifaa vya ujenzi huo vyenye thamani ya sh. milioni 12 yakiwemo mabati 200, wilayani humo, Meneja wa NMB, Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema pamoja na vifaa hivyo wametoa kompyuta mbili zenye thamani ya sh. milioni mbili.

Alieleza sekta za elimu na afya nipo miongoni mwa sekta za kimkakati zinazopewa kipaumbele na benki kwa kuangaliwa kwa jicho la kipekee, hivyo msaada huo sehemu ya sh. bilioni mbili za asilimia moja ya faida ya mwaka uliopita.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Meja Eduard Gowele, alisema benki inavyojitoa kwa haraka kusaidia jitihada za serikali katika sekta za miundombinu, elimu na afya, inafundisha namna sahihi ya kutumia Programu ya CSR.

> **Benki inavyojitoa kwa haraka kusaidia jitihada za serikali katika sekta za miundombinu, elimu na afya, inafundisha namna sahihi ya kutumia Programu ya CSR...**
>
> Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Meja Eduard Gowele.

Alibainisha zaidi ya sh. milioni 420 zimetumika katika ujenzi wa miundombinu ya elimu wilayani Kibiti, jitihada ambazo zinapewa nguvu na benki hiyo.

Mkuu wa wilaya huyo, aliwataka walimu na wanafunzi wa shule hizo kuutumia msaada huo kuongeza ufanisi wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kukuza kiwango cha ufaulu, huku akiwapongeza wafanyakazi wa benki kwa misaada inayotokana na michango yao binafsi.